# HOTUBA YA MHESHIMIWA SAMIA SULUHU HASSAN, RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA KWENYE MKUTANO NA WAZEE WA DAR ES SALAAM
# MLIMANI CITY, TAREHE 7 MEI, 2021

*Mheshimiwa Mzee Salim Matimbwa, Mwenyekiti wa Wazee wa Mkoa wa Dar es Salaam;*

*Mheshimiwa Philip Mangula, Makamu Mwenyekiti wa CCM – Tanzania Bara pamoja na Viongozi wote wa CCM mliopo;*

*Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;*

*Mheshimiwa Kassim Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Viongozi wote wa Serikali mliopo;*

*Mheshimiwa Abubakar Mussa Kunenge, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam;*

*Ndugu Kate Kamba, Mkoa wa Dar es Salaam;*

*Waheshimiwa Viongozi wa Kamati ya Usalama ya Mkoa wa Dar es Salaam;*

*Wazee wangu wa Mkoa wa Dar es Salaam;*

*Ndugu Wananchi, Wana-Habari, Mabibi na Mabwana:*

## NAWASALIMU KWA JINA LA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## SALAMU

Napenda nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, Muumba wetu, aliyetujalia uhai na kutuwezesha kukutana hapa leo tukiwa wenye afya njema. Aidha, naishukuru na kuipongeza Kamati ya Uratibu ya Mkutano huu, ikiongozwa na Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, kwa maandalizi yenu mazuri. Ahsanteni sana.

Kwa namna ya pekee sana, nawashukuru Wazee wangu wa Mkoa huu wa Dar es Salaam, ambao kimsingi, mnawakilisha Wazee wa nchi nzima, kwa kujitokeza kwenu kwa wingi kwenye Mkutano huu. Hii inaonesha kuwa mnaiunga mkono Serikali yenu. Ahsanteni sana wazee wangu. Binafsi, nataka niwashukuru sana wazee wangu kwa jinsi ambavyo mmeniunga mkono wakati wote tangu nikiwa Makamu wa Rais na sasa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; baada ya kifo cha aliyekuwa Rais wetu mpendwa, Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli. Na kwa sababu hiyo, naomba sote tusimame kwa dakika

moja tumwombee. Mwenyezi Mungu ailaze roho yake mahali pema peponi. Amina.

Kabla sijaendelea zaidi, napenda, hapa mwanzoni kabisa, niwaeleze jambo moja Wazee wangu. Kama mlivyoshuhudia, leo tumekutana tukiwa kwenye hali isiyo ya kawaida. Sote tumevaa barakoa. Hii inatokana na hali tuliyonayo sasa ya kuwepo kwa mlipuko wa ugonjwa wa UVIKO-19, ambao unawaathiri zaidi wazee. Hivyo basi, ili kuwakinga na kwa kuwa tumekusanyika kwa wingi, imetulazimu sote tuvae barakoa. Hivyo basi, nawaomba sana wazee wangu mtuwie radhi kwa kuleta utaratibu huu mpya; lakini ni kwa nia njema.

***Ndugu Wazee pamoja na Watanzania Mnaonisikiliza;***

Kama alivyosema Mheshimiwa Waziri wa Afya, nchi yetu ina takriban wazee **milioni 2.5** hii sasa. Hii maana yake ni kwamba Wazee ni kundi muhimu sana hapa nchini. Lakini kama hiyo haitoshi, na kama sote tujuavyo, kila mwanadamu mwenye kujaliwa umri na Mwenyezi Mungu, inafika wakati anakuwa mzee. Uwe unapenda au hupendi. Na katika hilo, kikawaida, mtu anahesabika kuwa mzee kuanzia miaka 60. Kwa hiyo, maana yake, hata mimi pia

tayari nimeshakuwa mzee; japokuwa hapo wapo wazee wengi walionizidi umri na maarifa.

Ni kwa kuzingatia hayo yote, nimeona ni vyema hapa mwanzoni kabisa mwa Uongozi wangu, nipate fursa ya kukutana nanyi wazee wangu. Hii ni kwa sababu uzee ni dawa. Wazee mmeona mengi na wana uzoefu mkubwa wa mambo. Hivyo basi, ni imani yangu kuwa, kupitia Mkutano huu, mimi na wenzangu Serikalini, tutapata mambo mengi ambayo yatanisaidia kwenye Uongozi wa Taifa letu.

Na katika hilo, napenda pia kutumia fursa hii kueleza ni kwa nini nimeamua kuzungumza na wazee wa Tanzania, kupitia ninyi wazee wa Dar es Salaam. Namshukuru Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa amezieleza baadhi ya sababu vizuri. Kwanza, Dar es Salaam ni Jiji lenye watu wa maeneo yote ya nchi yetu. Kwa hiyo, ukiongea na watu wa Dar es Salaam, una uhakika kuwa unaongea na Watanzania wote. Pili, ni kuendeleza utamaduni ulianzishwa tangu nchi yetu imepata Uhuru, Viongozi wetu walikuwa na utaratibu wa kuongea na Wazee wa Dar es Salaam, pindi wanapotaka kueleza jambo kubwa la kitaifa. Lakini, mimi leo sina

jambo, zaidi ya kutaka tu kuzungumza na ninyi wazee: Niwasikilize, mnielekeze na hatimaye nikayafanyie kazi.

Jambo jingine lililonisukuma kuja kuzungumza nanyi wazee wa Dar es Salaam ni kwamba, miezi michache iliyopita nilikuwa Mlezi wa Chama kwenye Mkoa huu, ambapo nimeulea kwa takriban miaka mitatu hadi minne hivi. Na nashukuru, ulezi wangu umelipa. Kwenye Uchaguzi Mkuu uliopita, Chama chetu kilifanikiwa kupata ushindi mkubwa. Hivyo, nawashukuru sana.

***Ndugu Wazee na Watanzania mnaonisikiliza;***

Baada ya maneno hayo ya utangulizi, naomba sasa niseme machache kuhusu Risala tuliyoisikiliza hivi punde. Kwanza kabisa, nawapongeza kwa Risala nzuri ambayo sio tu imesheheni mambo mengi bali pia imeandikwa kwa umaridadi mkubwa. Na katika hilo, napenda niwashukuru Wazee wangu kwa pongezi mlizonipatia kufuatia kupewa dhamana ya kuliongoza Taifa letu na pia kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Chama changu, Chama Cha Mapinduzi (CCM). Ahsanteni sana.

Lakini mbali na pongezi, kwenye Risala yenu mmeeleza baadhi ya changamoto zinawakabili na kuwasilisha maombi mbalimbali. Namshukuru Mheshimiwa Waziri wa Afya amezitolea majibu lakini naomba nami nizitolee maelezo. Kwanza ni kuhusu **Tiba kwa Wazee**. Mmeeleza kwamba kuna shida kwenye kupata baadhi ya vipimo na dawa; na kwamba Kadi za Msamaha wa Matibabu hazikubaliki kwenye Hospitali za Rufaa. Changamoto hii ni ya msingi na ni ya kweli. Pamoja na maelezo ya Mheshimiwa Waziri wa Afya, nami nataka nieleze kuwa suala la tiba katika ngazi yoyote ni haki yenu ya msingi. Hivyo basi, napenda niwahakikishie kuwa, katika marekebisho ya Sera tunayokwenda kuyafanya, na kwa kuzingatia maelekezo ya Ilani yetu ya Uchaguzi, tutalizingatia ili kuwaondolea shida na kero mnazopata.

kwa hatua za awali, naziagiza Wizara za TAMISEMI na Wizara ya Afya kushirikiana katika kuimarisha upatikanaji wa dawa na wataalam wabobezi wa magonjwa ya wazee, hususan kwenye Hospitali za ngazi ya Halmashauri. Aidha, naiagiza Wizara ya Afya kuliangalia

suala la Vitambulisho au Kadi za Matibabu ya Wazee. Kama nilivyosema awali, sisi sote ni wazee watarajiwa.

Aidha, kuhusu suala la tiba kwa wazee, kama nilivyogusia awali, hivi sasa dunia ipo kwenye janga la Corona. Waathirika wakubwa wa ugonjwa huu ni watu wenye umri mkubwa. Kwa kutambua hilo, napenda kuwaarifu Wazee wangu kuwa tumeunda Kamati Maalum kwa ajili ya kuleta mapendekezo Serikalini kuhusu namna ya kukabiliana na ugonjwa huu. Wakati tunasubiri mapendekezo ya Kamati hiyo, nataka niwaahidi Wazee wangu kuwa, yale yote yanayowafanya wazee kuwa kwenye kundi hatarishi zaidi, tutayashughulikia kwa kuwakinga na pia kuwapa mbinu za kujikinga.

Changamoto pili ni kuhusu **Sheria Inayowahusu Wazee**. Lakini, kama mnavyofamu, Sheria inaanza na Sera, na kama mlivyosikia, Serikali imeanza kufanya mapitio ya Sera ya Wazee ya Mwaka 2003 ili iendane na mazingira ya sasa. Utayarishaji wa Sera hiyo mpya utakapokamilika, ambapo tutanatarajia itakuwa mwaka huu, mara moja tutatunga Sheria ili kuipa nguvu Sera itakayopitishwa.

Tatu, ni kuhusu **Uwezeshaji wa Wazee Kiuchumi**, ikiwemo kupata mikopo isiyo na riba. Ningependa kusema kuwa, Serikali imekuwa ikijitahidi kwa kadri ya uwezo wake kuwawezesha wazee kiuchumi. Mathalan, kupitia Mpango wa TASAF, hivi sasa, tunatoa ruzuku kwa wazee wapatao **476,313** kila mwezi. Na kuanzia mwaka huu, Mfuko huu utafanya kazi kwenye Wilaya zote. Zaidi ya hapo, Serikali imeanza kuandaa Mradi mpya utakaochukua nafasi ya TASAF ambayo itafikia ukomo hivi karibuni. Kwa upande mwingine, tutaendelea kutoa pensheni kwa wazee wastaafu walioitumikia Serikali. Lakini kuhusu suala la kutaka wazee wote kupewa pensheni; nataka niwe mkweli, kutokana na uwezo wetu wa sasa, itakuwa vigumu kutekeleza suala hilo kutokana na mdororo wa uchumi na pia miradi mingi mikubwa ya kimkakati tunayoitekeleza. Hivyo basi, nawasihi wazee wangu mtuvumilie.

Nne; **Uwakilishi wa Wazee kwenye Vyombo vya Maamuzi**, hususan kwenye Mabaraza ya Madiwani na Bunge. Ni kweli jambo hili ni la msingi sana. Kuna umuhimu mkubwa wa wazee kuwemo kwenye vyombo hivyo sio tu ili kutetea maslahi yao bali pia ili kunufaika na

uzoefu wao. Kama nilivyosema awali, **"***Uzee ni dawa*"; na vilevile, kule Zanzibar kuna usemi *"Isiyo Kongwe Haivushi"*. Hii ndiyo sababu zimekuwepo fursa mbalimbali za kuwawezesha wazee kuingia kwenye vyombo hivyo vya maamuzi. Na katika hilo, nakipongeza Chama changu (CCM) ambacho, kupitia marekebisho ya Katiba yaliyofanyika hivi karibuni, kimetambua nafasi ya Wazee. Zaidi ya hapo, CCM imetenga nafasi mbili za Ubunge kwa wazee; na nataka niahidi kuwa, penye majaliwa, siku zijazo tutaliangalia zaidi.

Tano, **Makazi kwa Wazee Wasiojiweza**: Ni kweli kabisa kuwa kutokana na sababu mbalimbali, ikiwemo kutelekezwa, wapo wazee wengi ambao hawana makazi. Serikali imekuwa ikijitahidi kujenga au kuboresha makazi kwa ajili ya wazee wa namna hiyo. Mathalan, kwenye miaka mitano iliyopita, Serikali tumeboresha makazi ya wazee Kolandoto (Shinyanga), Nunge (Dar es Salaam), Njoro (Kilimanjaro), Magugu (Manyara), pamoja na Fungafunga (Morogoro). Nataka niahidi kuwa tutaendelea kujenga na kuboresha makazi ya wazee.

Lakini, pamoja na hatua hizo, nataka niseme kuwa hili si jambo ninalopenda sana. Na hii ni kwa sababu, ninafahamu, wazee hawa wana watoto ama ndugu na jamaa. Kwa hiyo, itapendeza zaidi endapo wazee hawa wakilelewe na watoto ama ndugu zao. Hivyo basi, nitoe wito kwa jamii ya Kitanzania tuwatunze wazee wetu.

Sambamba na hilo, ni kuhusu kero ya **Huduma kwenye Usafiri wa Vyombo vya Umma**. Suala hili nalo ni la kimaadili zaidi. Na hii ni kwa sababu, endapo mtoto atakuwa amelelewa vizuri, akiingia kwenye basi hawezi kukubali kumwona mzee amesimama na yeye amekaa kwenye kiti. Kinyume chake ujue kuna dosari mahali. Hivyo basi, natoa wito kwa Watanzania wenzangu, hususan wazazi, kujitahidi kuwalea watoto wetu kwenye maadili mema. Na hili nalisema nikiwa na mfano halisi. Kwenye magari yetu ya Mwendokasi, kuna viti maalum vimetengwa kwa wazee na watu wenye shida mbalimbali, (*wajawazito, wagonjwa*). Lakini, inashangaza kukuta vijana wamekaa kwenye kiti huku wazee wakiwa wamesimama. Hii ndiyo sababu nahimiza sana Watanzania tuwalee watoto wetu kwenye maadili mema. Lakini, nitumie fursa

hii pia kutoa rai kwa makondakta nao kuhakikisha wanasimamia suala hili kwenye vyombo vyao. Naamini, yote hayo yakifanyika, hatatukuwa na sababu ya kuwa vyombo vya usafiri maalum kwa ajili ya wazee.

***Ndugu Wazee Wangu;***

Kwa ujumla, kama nilivyosema awali, changamoto na maombi yote mliyoyawasilisha ni ya msingi. Hivyo basi, Serikali tumeyapokea na tutajitahidi kuyashughulikia. Na kwa bahati nzuri, masuala karibu yote mliyoeleza yamo kwenye Ilani yetu ya Uchaguzi ya Mwaka 2020 – 2025 na pia tumeyajumuisha kwenye Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano, ambao utekelezaji wake tutauanza mwezi Julai 2021.

***Waheshimiwa Wazee Wangu;***

Kabla sijahitimisha hotuba yangu, naomba mniruhusu nieleze baadhi ya masuala machache kuhusu Serikali. Kama mtakavyokumbuka, tarehe 22 Aprili, 2021 nilipata fursa ya kuhutubia Bunge letu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwenye Hotuba hiyo, nilieleza vipaumbele vya Serikali ya Awamu ya Sita; na kwa haraka haraka, naomba nitaje baadhi ya vipaumbele hivyo:

Kwanza, **kudumisha Amani na Usalama**. Kama mnavyofahamu, amani na usalama ni msingi wa maendeleo. Bila ya amani hakuna maendeleo; na zaidi, pasipo na amani, wenye kuathirika zaidi ni pamoja na wazee. Na kuhusu hilo, katika siku za hivi karibuni, kumeibuka vitendo vya ujambazi, hususan hapa Dar es Salaam. Kuna watu wanajaribu kina cha maji. Natoa onyo kwa watu hao kuwa wasijaribu kina cha maji. Na hapa nataka kumuagiza Inspekta Jenerali wa Polisi kuhakikisha anakomesha vitendo hivyo. Zaidi ya hapo, nirudie wito wangu kwa wazee na wazazi kusimamia maadili kwa watoto wetu.

Sambamba na kudumisha amani na usalama, kipaumbele kingine ni **kulinda uhuru**, **Muungano wetu, Mshikamano, pamoja na Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar**. Mambo haya hayana mbadala. Hivyo, tutaendelea kuyaenzi, kuyatunza na kuyaendeleza.

Tatu, tumeahidi **Kuendeleza Jitihada za Kukuza Uchumi**: Na hapa tutaendeleza kazi nzuri zilizoanza kutekelezwa na Awamu zote zilizotangulia, ikiwemo ujenzi wa miundombinu ya usafiri na huduma za usafirishaji.

Lengo likiwa ni kuchochea ukuaji uchumi nchini. Kama mnavyofahamu, licha ya kuingia uchumi wa kati, bado tuna kazi kubwa ya kufanya.

Na hapa nataka niseme kuwa, kila Mtanzania ana wajibu wa kutoa mchango wake katika kujenga uchumi bila kujali tofauti zetu za jinsia, rangi, kabila, dini au itikadi za vyama. Nasema hivyo kwa sababu, huko mbeleni, katika kupanga safu za uongozi, sitazingatia mambo hayo. Nitamchagua Mtanzania yeyote mwenye sifa kwa kuzingatia weleni na kuleta umoja wa kitaifa.

Tutaendelea pia na **Uboreshaji wa Huduma za Kijamii**, ikiwemo kutoa elimu bila malipo na kuboresha upatikanaji wa huduma za afya na maji. Na kuhusu maji, naupongeza Mkoa wa Dar es Salaam kwa kutekeleza miradi mikubwa ya maji (Kimbiji na Mpera), ambapo itakapokamilika, itamaliza kabisa tatizo la maji katika Jiji hili. Na katika hilo, narudia agizo langu kwa Wizara ya maji kuacha tabia ya kubambikiza bili za maji. Lakini, niwaombe pia wananchi, kulipia bili za maji ili tuweze kutoa huduma za maji kwa Watanzania wengine.

Tutaboresha pia upatikanaji wa nishati, kwa ajili ya ujenzi wa viwanda na vilevile kuuza nje. Hivi karibuni, nilienda Kenya, ambao wametuomba tuwauzie gesi. Zaidi hapo, tunakusudia kuboresha huduma ya mawasiliano, ambapo tunakusia kufikisha Mkonga wa Taifa kwenye maeneo mengi ya nchi yetu. Kwa hapa Dar es Salaam, tutaendelea na ujenzi wa barabara na madaraja ya juu kama tulivyoahidi kwenye Ilani yetu ili kupunguza kama sio kumaliza kabisa tatizo la msongamano.

Sita, **Usimamiaji Haki, Uhuru na Demokrasia**. Tutajitahidi sana kuheshimu haki za binadamu na kulinda uhuru wa watu na pia vyombo vya habari. Na ninyi wenyewe ni mashahidi wa hatua ambazo tumeanza kuzichukua kwenye eneo la kodi.

Saba, **Uhusiano wa Kimataifa**, ambapo tunakusudia kuimarisha uhusiano na mataifa jirani, uhusiano wa Kikanda na Kimataifa. Na katika hilo, kama mnavyofahamu, tayari nimefanya ziara kwenye nchi mbili (Kenya na Uganda) za kujitambulisha.

Ili kuweza kutimiza hayo yote, nawasihi Wazee wangu kuwa, huko mbeleni mtarajie kuona mabadiliko katika nyanja mbalimbali. Na lengo la mabadiliko hayo ni kutengeneza na siyo kubomoa. Miongoni mwa mabadiliko tutakayofanya yatakuwa ya kitaasisi, kimuundo na pia Uongozi. Hivyo basi, nawaomba sana Wazee wangu mtuunge mkono ili tuweze kutimiza dhamira tuliyonayo ya kuiletea maendeleo nchi yetu. Endapo mtaona tunatetereka, msisite kutukumbusha ili turudi kwenye mstari. Tutasikiliza bila bezo au dharau yale yote mtakayotueleza; na tutatekeleza yale yatakuwa ndani ya uwezo wetu kwa wakati husika. Na katika hilo, nawasihi pia wazeee wangu mwendelee kuwahimiza wananchi kuendelea kudumisha amani, kuchapa kazi kwa bidii na bila kusahau kulipa kodi; kwa sababu kodi ndiyo maendeleo yetu.

Zaidi ya hapo, kama nilivyosema awali, wazee hamna budi kuendelea kuhimiza malezi bora kwa vijana wetu. Mimi naamini, vijana wetu wakilelewa vizuri, sio tu hatutakuwa na ulazima wa kutenga viti maalum kwenye vyombo vya usafiri bali pia tutajenga Taifa la watu waadilifu, waaminifu na uzalendo kwa nchi lao;

wasiojihusisha na vitendo viovu vya wizi, rushwa, matumizi ya dawa za kulevya na vitendo vingine ambavyo ni kinyume cha maadili na tamaduni zetu.

Nihitimishe kwa kurudia tena kuwashukuru Wazee wangu kwa kujitokeza kwenu kwa wingi kwenye Mkutano huu. Baada ya kusema hayo, narudia nawasalimu tena kwa Jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**"Ahsanteni sana kwa kunisikiliza"**